TANGAZO LA SERIKALI NA. 384 lililochapishwa tarehe 2/6/2023]

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA

(SURA YA 415)

# KANUNI

KANUNI ZA USAJILI WA WASAFIRISHAJI KWA NJIA YA MAJI ZA MWAKA, 2023

*Tangazo La Serikali Na. 384 (Linaenedelea)*

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA
(SURA 415)

KANUNI

*(Zimeandaliwa chini ya kifungu cha 12(1)(k) na 61)*

# KANUNI ZA USAJILI WA WASAFIRISHAJI KWA NJIA YA MAJI ZA MWAKA, 2023

MPANGILIO WA KANUNI

SEHEMU YA I
VIFUNGU VYA AWALI

| *Kanuni* | *Jina* |
|---|---|
| 1. | Jina la Kanuni. |
| 2. | Matumizi. |
| 3. | Tafsiri. |

SEHEMU YA II
MAOMBI YA USAJILI NA UTOAJI
CHETI CHA USAJILI

| | |
|---|---|
| 4. | Maombi ya usajili. |
| 5. | Kustahiki na matakwa ya usajili. |
| 6. | Uamuzi wa maombi. |
| 7. | Utoaji au kukataa kutoa cheti.. |
| 8. | Kutohamishwa kwa cheti. |
| 9. | Rejista ya Wasafirishaji. |
| 10. | Uhalali wa usajili. |
| 11. | Kuhuisha usajili. |
| 12. | Kupoteza cheti. |
| 13. | Mabadiliko ya taarifa. |
| 14. | Uwasilishaji wa nyaraka. |

SEHEMU YA III
WAJIBU NA HAKI YA MSAFIRISHAJI

15. Wajibu wa msafirishaji.
16. Haki za msafirishaji.

SEHEMU YA IV
VITENDO VILIVYOKATAZWA NA USIMAMIZI WAKE

17. Vitendo vilivyokatazwa.
18. Ufuatiliaji.
19. Notisi ya kurekebisha.
20. Kufutiwa usajili wa msafirishaji.
21. Ushughulikiaji wa malalamiko.

MAJEDWALI

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA
(SURA 415)

KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 12(1)(k) na 61)*

# KANUNI ZA USAJILI WA WASAFIRISHAJI KWA NJIA YA MAJI, 2023

## SEHEMU YA KWANZA

## MASHARTI YA AWALI

Jina

1.Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Uwakala wa Meli Tanzania (Usajili wa Wasafirishaji kwa Njia ya Maji), 2023.

Matumizi

2.Kanuni hizi zitatumika kwa msafirishaji wa Tanzania Bara isipokuwa msafirishaji wa mizigo binafsi, shehena ya kidiplomasia, shehena ya serikali, shehena ya msaada, shehena iliyosafirishwa nje ya nchi kutokana na kazi ya Serikali.

Tafsiri

3.Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo-

Sura 415

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;

“afisa aliyeidhinishwa” maana yake ni mfanyakazi wa Shirika aliyepewa jukumu la kuhudumia jambo lolote linalohusiana na utekelezaji wa Kanuni hizi;

“mzigo” maana yake ni bidhaa zilizotengwa kwa ajili ya kusafirishwa kupitia mpaka wa forodha;

"cheti" maana yake ni hati ya usajili wa msafirishaji wa shehena kinachotolewa kwa msafirishaji aliyesajiliwa na Shirika kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi;

Sura 415

"Shirika" ina maana iliyoainishwa kwenye Sheria;

T.S Na. 358 la 2012

"bidhaa hatarishi" ina maana iliyoainishwa kwenye Kanuni za Usafirishaji kwa Njia ya Maji (Bidhaa Hatari na Vichafuzi vya Baharini);

T.S Na. 197 la 2016

"uzito wa jumla" ina maana iliyoainishwa kwenye Kanuni za Usafirishjai kwa Njia ya Maji (Uzito wa Jumla uliothibitishwa wa Kontena la Kubebea Mizigo);

T.S Na. 197 la 2016

"kifurushi" ina maana iliyoainishwa kwenye Kanuni za Usafirishjai kwa Njia ya Maji (Uzito wa Jumla uliothibitishwa wa Kontena la Kubebea Mizigo);

Sura 415

"huduma inayodhibitiwa" ina maana iliyoainishwa kwenye Sheria;

Sura 415

"mtoa huduma anayedhibitiwa" ina maana iliyoainishwa kwenye Sheria;

Sura 415

"msafirishaji" ina maana iliyoainishwa kwenye Sheria; na

T.S Na. 197 la 2016

"uzito wa jumla iliothibitishwa" ina maana iliyoainishwa kwenye Kanuni za Usafirishjai kwa Njia ya Maji (Uzito wa Jumla uliothibitishwa wa Kontena la Kubebea Mizigo).

## SEHEMU YA PILI
## USAJILI WA WASAFIRISHAJI KWA NJIA YA MAJI

Kustahiki na matakwa ya usajili

4–(1) Mtu atastahili kuomba usajili iwapo ni msafirishaji kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Msafirishaji anayeomba kusajiliwa atatakiwa-

(a)ikiwa ni shirika au ubia, kuambatisha pamoja na maombi nakala iliyoidhinishwa ya-

(i)leseni ya biashara;

(i) cheti cha Nambari ya Utambulisho wa

Mlipakodi;

(ii) cheti cha uandikishwaji, cheti cha uzingatiaji au cheti cha usajili; na

(iii) nyaraka nyingine zozote kama zitakavyohitajika na Shirika;

(a) iwapo ni mtu binafsi, kuambatisha pamoja na maombi nakala iliyoidhinishwa ya-

(i) leseni ya biashara;

(ii) cheti cha Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi;

(iii) kitambulisho cha Taifa au Pasi ya kusafiria; na

(iv) nyaraka nyingine zozote kama zitakavyohitajika na Shirika.

Maombi ya usajili

5.Maombi ya usajili yatawasilishwa kwa Shirika kwa kutumia fomu iliyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza, na itaambatishwa na uthibitisho wa malipo ya ada kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili.

Uamuzi wa maombi

6.Shirika, baada ya kupokea ombi lililowasilishwa kwa mujibu wa kanuni ya 5, litatoa uamuzi wa ombi hilo.

Utoaji au kukataa kutoa cheti.

7.-(1) Baada ya kupokea maombi ya usajili, Shirika litafanya uamuzi wa kutoa au kukataa kutoa usajili.

(2) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1), iwapo Shirika limejiridhisha kwamba mleta maombi amekidhi matakwa yote ya usajili, Shirika linaweza, ndani ya siku saba za kazi kuanzia tarehe ya kupokea ombi la usajili, kutoa cheti cha usajili kwa namna iliyoainishwa kwenye Jedwali la Tatu.

(3) Iwapo Shirika limejiridhisha kwamba mleta maombi ameshindwa kukidhi matakwa ya usajili kama

yalivyoainishwa kwenye Kanuni hizi, Shirika litatoa notisi ya kukataa kutoa usajili katika namna iliyoainishwa kwenye Jedwali la Nnne..

(4) Mleta maombi aliyekubaliwa anaweza anaweza kuchukua cheti kilichotiwa saini kutoka kwa ofisi yoyote ya Shirika au kukichapisha mtandaoni.

Kutohamishwa kwa cheti

8.Cheti kilichotolewa chini ya Kanuni hizi hakitahamishwa.

Rejista ya wasafirishaji

9.(1) Shirika litaanzisha na kutunza rejista ya wasafirishaji katika muundo ulioainishwa katika Jedwali la Tano.

(2) Shirika litahakikisha kuwa Rejista ya Wasafirishaji inapatikana mtandaoni kwa ajili ya umma.

Uhalali wa usajili

10.Cheti kilichotolewa chini ya Kanuni hizi kitakuwa halali kwa muda wa miaka mitatu kuanzia tarehe ya kutolewa na usajili huo unaweza kuhuishwa.

Kuhuisha usajili

11.–(1) Msafirishaji anayekusudia kuhuisha usajili atatuma maombi katika fomu iliyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza, na fomu hiyo itaambatishwa na uthibitisho wa malipo ya ada iliyoainishwa kwenye Jedwali la Pili..

(2) Masharti yanayohusiana na maombi ya usajili wa kwanza yatatumika kwa ajili ya maombi ya kuhuisha usajili chini ya kanuni hii.

Kupoteza cheti

12.-(1) Pale cheti kilichotolewa chini ya Kanuni hizi kinapopotea au kuharibiwa, msafirishaji-

(a) ataliomba Shirika nakala iliyodurufiwa katika namna iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza;

(b) ataomba na kuambatanisha katika maombi hayo taarifa ya upotevu ya polisi na nyaraka nyingine yoyote kama itakavyohitajika na Shirika; na

(c) atalipa ada kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), Shirika baada ya kupokea maombi ya nakala ya cheti na kujiridhisha juu ya maombi hayo, litatoa nakala ya cheti katika namna iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu..

Mabadiliko ya Taarifa

13.-(1) Pale ambapo msafirishaji anabadilisha taarifa zozote za msingi zilizowasilishwa kwa Shirika chini ya Kanuni hizi, atatakiwa ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya mabadiliko hayo, kutoa taarifa kwa Shirika kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Sita.

(2) Shirika, baada ya kupokea mabadiliko ya taarifa, litafanya mabadiliko hayo kwenye Rejista ya wasafirishaji.

Uwasilishaji wa nyaraka

14.Nyaraka yoyote inayotakiwa kuwasilishwa kwa Shirika chini ya vifungu vya Kanuni hizi inaweza kuwasilishwa katika muundo na namna ambayo inajumuisha njia ya kielektroniki kwa kadiri Shirika litakavyoona inafaa.

## SEHEMU YA TATU
## WAJIBU NA HAKI ZA MSAFIRISHAJI

Wajibu wa msafirishaji

15.Msafirishaji ana wajibu wa-

(a) kuhakikisha kwamba hatua zinazofaa za tahadhari ya usalama wa mzigo zinachukuliwa kabla ya kusafirishwa;

(b) kufungasha vyema na kuweka alama mizigo kwa mujibu wa viwango vya usalama vilivyowekwa na sheria husika;

(c) kuandaa ipasavyo, kuweka alama za kutosha, kuweka kumbukumbu kwa usahihi na kuweka lebo kwenye bidhaa hatarishi ili kuzifanya kuwa salama kwa ajili ya kubebwa, kuhifadhiwa na

kusafirishwa kwa mujibu wa sheria husika;

(d) kuhakikisha kwamba bidhaa zinazoharibika zimefungwa vizuri, zimewekwa alama na kushughulikiwa kwa mujibu wa mahitaji ya uhifadhi wake;

(e) kuhakikisha shehena itakayosafirishwa iko katika hali nzuri na inastahili kubebwa;

(f) kuzingatia utaratibu wa kiutawala kama unavyobainishwa mara kwa mara na mwendesha bandari au bandari kavu;

(g) kupata cheti cha uthibitisho wa uzito wa jumla wa kontena lililopakiwa kabla ya kupakiwa kwenye meli kwa ajili ya kusafirishwa nje ya nchi;

(h) kuwasiliana na kuwasilisha cheti cha uthibitisho kwa wakala wa meli na mwendeshaji wa bandari ili kuwezesha mpango sahihi wa upakiaji wa meli;

(i) kutoa taarifa za mizigo ikijumuisha maelezo ya shehena, asili, uzito, hali, wingi na ubora, bandari ya kupakia, bandari ya kupakua au taarifa nyingine yoyote kama itakavyohitajika na mamlaka husika;

(j) kujiepusha kutumia watu wasioidhinishwa katika kushughulikia shehena zake; na

(k) kutoa taarifa, kutoa nyaraka au ushahidi kama itakavyotakiwa na Shirika.

Haki za msafirishaji

16.-(1) Msafirishaji atakuwa na haki ya -

(a) kualikwa au kuhusishwa moja kwa moja au kupitia uwakilishi katika programu husika za kujenga uwezo zinazoandaliwa na Shirika;

*Tangazo La Serikali Na. 384 (Linaenedelea)*

(b) kutambulishwa kwa wahusika wengine kwa nia ya kuwezesha biashara ya meli na usafirishaji wa mizigo;

(c) kushirikishwa ili kupata maoni kuhusu masuala husika katika sekta ya usafiri kwa njia ya maji;

(d) kupatiwa maamuzi ya kiudhibiti na taarifa kuhusu masuala muhimu kwa wasafirishaji; na

(e) kupata taarifa zinazotolewa kuhusiana na sheria za usafiri kwa njia ya maji, viwango, gharama na ada zinazotumika.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), msafirishaji atakuwa na haki ya kuwasilisha kwa Shirika lalamiko lolote dhidi ya mtoa huduma anayedhibitiwa kwa njia iliyoainishwa chini ya Sheria.

## SEHEMU YA NNE
## VITENDO VILIVYOKATAZWA NA USIMAMIZI WAKE

Vitendo vilivyokatazwa

17.-(1) Msafirishaji –

(a) hatatoa taarifa za uongo au za kupotosha kuhusiana na usafirishaji wa mizigo;

(b) atajiepusha na vitendo vya kugushi, rushwa na shughuli haramu;

(c) hatotenda kwa namna isiyofaa kwa wahusika wengine au kwa sifa ya sekta ya usafiri kwa njia ya maji;

(d) hatohodhi vifaa vya wahusika wengine kinyume na masharti yaliyokubaliwa baina ya pande husika;

(e) hatofanya ghiliba kwenye shehena yake au ya watu wengine au kusababisha upungufu wa

shehena hiyo ili kupata faida isiyo ya haki dhidi ya wahusika wengine katika msururu wa usafiri kwa njia ya maji;

(f) hatoshirikiana na upande wowote kwa nia ya kukiuka masharti ya Kanuni hizi au sheria yoyote husika katika sekta ya usafiri kwa njia ya maji;

(g) hatokosa kuwa mwaminifu wakati wa kushughulika na wahusika wengine na wakati wa kushughulikia suala lolote la maslahi ya kibiashara au kifedha katika sekta ya usafiri kwa njia ya maji;

(h) hatowatendea wahusika wengine bila utu, heshima na adabu; na

(i) hatofanya kazi bila cheti halali cha usajili.

(2) Mtu anayekiuka masharti ya kanuni ndogo (1) anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na hamsini lakini isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.

Ufuatiliaji

18.-(1) Shirika linaweza kumfuatilia msafirishaji aliyesajiliwa kwa madhumuni ya kuhuisha maelezo katika Rejista ya wasafirishaji na kukusanya maoni kuhusu ubora wa huduma zinazodhibitiwa.

(2) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1), Shirika linaweza, wakati wa kufanya ufuatiliaji, kutafuta taarifa kutoka kwa mamlaka yoyote au kumtaka msafirishaji kutoa taarifa, kumbukumbu, maelezo au nyaraka zinazohusiana na usajili.

Notisi ya kurekebisha

19. Kwa kuzingatia kanuni ya 19, Shirika linaweza kutoa notisi ya maandishi inayomtaka msafirishaji kurekebisha mapungufu yoyote yaliyobainika ndani ya muda ulioainishwa katika notisi kwa kuzingatia Jedwali la

Saba.

Kufutiwa usajili wa msafirishaji

20.(1) Iwapo msafirishaji-

(a) Anatumia vibaya au anafanya ubadhirifu wa vifaa vya wahusika wengine;

(b) anatoa taarifa za uongo au kupotosha kuhusiana na usafirishaji wa mizigo;

(c) anatenda kwa namna isiyofaa kwa wahusika wengine au kwa sifa ya sekta ya usafiri kwa njia ya maji; au

(d) anashindwa kurekebisha mapungufu ya usajili ndani ya muda ulioainishwa kwenye notisi ya urekebishaji,

Shirika litatuma notisi kwa msafirishaji, kupitia anwani yake ifaayo katika namna iliyoainishwa katika Jedwali la Saba, ikimtaka kurekebisha upungufu uliobainika ndani ya siku ishirini na moja kuanzia tarehe ya taarifa.

(2) Baada ya kuisha kwa muda ulioainishwa kwenye kanuni ndogo ya (1), Shirika linaweza kutuma kwa msafirishaji notisi ya pili na baada ya kumalizika kwa siku thelathini kutoka tarehe ya notisi, jina la msafirishaji lililoandikwa kwenye notisi, isipokuwa kama kuna sababu za msingi za kulishawishi Shirika kuamua vinginevyo,, litafutwa kwenye Rejista ya wasafirishaji.

(3) Notisi itachukuliwa kuwa imetolewa ipasavyo kwa msafirishaji kwa-

(a) kutoa notisi kwa njia ya kukabidhi kwa mkono;

(b) kutuma barua kwenye anuani iliyosajiliwa;

(c) kubandikwa na kusomeka katika eneo dhahiri la

msafirishaji lililosajiliwa; au

(d) kutuma kupitia anwani ya barua pepe iliyosajiliwa ya msafirishaji aliyesajiliwa.

Ushughulikiaji wa malalamiko
GN. Na. 338 ya 2018

21.Msafirishaji ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa Shirika uliotolewa chini ya Kanuni hizi au kitendo cha mtoa huduma anayedhibitiwa anaweza kutafuta suluhu kwa mujibu wa Kanuni za Uwakala wa Meli Tanzania (Ushughulikiaji wa Malalamiko).

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA
TASAC

JEDWALI LA KWANZA

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni 5(1), 12(1) na 13(1)(a))*

OMBI LA CHETI CHA MSAFIRISHAJI

Aina ya Msafirishaji: Kampuni ☐ Mtu binafsi ☐ Ubia ☐

1. Jina la mwombaji: ……………………....................................................
2. Anuani ya posta:.....................................................................................
3. Na. Simu.: ....................Barua pepe: ………………….................................
4. Cheti cha uandikishwaji/uzingatiaji/usajili: ................................. Tarehe ya kutolewa:……………………
5. Cheti cha Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi…………....................
6. Namba ya leseni ya biashara: …………........................................................
7. Namba ya kitambulisho cha taifa/pasi ya kusafiria…........................

*Tangazo La Serikali Na. 384 (Linaenedelea)*

8. Anuani ya makazi: Mtaa: ……………………….......... Namba ya kiwanja:…………………………….…….
   Nyumba/Namba ya jengo: ……………………………
   Wilaya:……………………………………………….
   Mkoa: ………………………………………………
9. Aina ya usajili: Mpya ☐ Huisha ☐ Nakala ☐
10. Namba ya cheti cha usajili wa awali. …………………….. Mwaka wa usajili wa awali…………

11. Kiwango cha mzigo uliosafirishwa au unaotegemewa kusafirishwa

| Aina ya bidhaa | Kiwango cha mzigo uliosafirishwa | | Kiwango cha mzigo unategemea kusafirishwa | |
|---|---|---|---|---|
| | Tani | Makasha | Tani | Makasha |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

**Unaweza kuingiza safu mlalo ya ziada iwapo kuna aina ya ziada ya usafirishaji*

*Kwa hili natangaza kwa ufahamu wangu na imani yangu kwamba taarifa zote zilizomo katika maombi haya ni za kweli na sahihi. Ninajitolea kuarifu mabadiliko yoyote katika maelezo yoyote yaliyotolewa hapo.*

*Jina kamili*.....................................................................................................................
Cheo: …………………………………………………………………………........
Saini: ………………………………… Tarehe:......…………………..................
(Muhuri)

KWA MATUMIZI YA OFISI

Pendekezo la Kuidhinishwa/Kukataliwa

Imependekezwa: Sababu:
1. Kuidhinishwa ☐
2. Kukataliwa ☐

Jina:..………………… Cheo: ………………......
Saini:………………… Tarehe:…………………

*Tangazo La Serikali Na. 384 (Linaenedelea)*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA

---

JEDWALI LA PILI

---

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 5(2), 12(2) and 13(1)(c))*

ADA ZA MAOMBI YA CHETI CHA MSAFIRISHAJI

| AINA YA HUDUMA | MAELEZO | KIASI (USD) |
|---|---|---|
| Kusajili au Kuhuisha cheti cha usafirishaji | Ada ya maombi: | |
| | Mtu binafsi | 5.00 |
| | Ubia | 10.00 |
| | Kampuni | 10.00 |
| Cheti Kimepotea/kuharibika | Ada ya nakala ya cheti | 5.00 |

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA
TASAC

---

JEDWALI LA TATU

---

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 8(1) na 13(2))*

Na. ya usajili: …………

CHETI CHA USAJILI WA MSAFIRISHAJI

Hii ni kuthibitisha kuwa:

M/s.: ……………………………………………………………… baada ya kukidhi matakwa ya usajili chini ya *Kanuni za Usajili wa Wasafirishaji kwa Njia ya Maji, 2023* anasajiliwa/inasajiliwa kama msafirishaji.

*Tangazo La Serikali Na. 384 (Linaenedelea)*

Mahali.............................. tarehe……… mwezi ........................... 20......

Inatumika hadi …………………………………………..

……………………………………..

MKURUGENZI MKUU

SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA
TASAC

JEDWALI LA NNE

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 8(2))*

NOTISI YA KUKATAA KUTOA CHETI CHA USAJILI WA MSAFIRISHAJI

Kwa M/S ……………………………………………………………………

1. Unaarifiwa kwamba maombi yako ya kusajiliwa kama msafirishaji chini ya Kanuni za Usajili wa Wasafirishaji kwa Njia ya Maji, yamekataliwa.

2. Sababu za kukataa ni kama ifuatavyo:

    (a) ...........................................................................................................
    (b) ...........................................................................................................
    (c) ...........................................................................................................
    (d) ...........................................................................................................

3. Hata hivyo, maombi yako yanaweza kuangaliwa upya chini ya masharti yafuatayo:

(a) ..........................................................................................................
(b) ..........................................................................................................
(c) ..........................................................................................................
(d) ..........................................................................................................

Mahali.................................. tarehe……… mwezi .................. 20......

……………………………………..

MKURUGENZI MKUU
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA

*Tangazo La Serikali Na. 384 (Linaenedelea)*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA
TASAC

## JEDWALI LA TANO

*(Imeandaliwa chini ya kanuni ya 10(1))*

## REJISTA YA WASAFIRISHAJI

| TAARIFA ZA MSAFIRISHAJI | | | | | | | | TAARIFA ZA USAJILI | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Na. | Jina la msafirishaji | TIN | Anwani ya posta | Na. ya simu | Barua pepe | Anwani ya makazi | Aina ya mzigo unaosafirishwa | Aina ya msafirishaji | Na. ya cheti cha usajili | Tarehe ya kutolewa | Tarehe ya kuisha matumizi |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA
TASAC

______

JEDWALI LA SITA

______

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 14(1))*

______

NOTISI YA MABADILIKO YA TAARIFA ZA MSAFIRISHAJI

Kwa: Mkurugenzi Mkuu,

Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC),

S.L.P 989,

DAR ES SALAAM.

Mimi;…………………………………………………………………………
……………………………… mwenye usajili wa cheti cha msafirishaji namba..............................................…………… kilichosajiliwa kwa mujibu wa matakwa ya ya *Kanuni za Usajili wa Wasafirishaji kwa Njia ya Maji, 2023*.

Ninatoa notisi kuwa, katika tarehe ............. ya mwezi.......................... 202..., mabadiliko yafuatayo yalitokea au yalifanyika, kuhusiana na maelezo yaliyosajiliwa katika Rejista ya Wasafirishaji ili kusomeka kama ifuatavyo-

(1) ..................................................................................................................
(2) ..................................................................................................................
(3) ..................................................................................................................
(4) ..................................................................................................................

Mahali...................................... tarehe……… mwezi ..................... 20......

*Tangazo La Serikali Na. 384 (Linaenedelea)*

Jina : …………………Cheo: …………………  Saini: ………………....

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI  NA UCHUKUZI
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA
TASAC

JEDWALI LA SABA

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni 20 na 21(1))*

NOTISI YA KUREKEBISHA MAPUNGUFU NA UKIUKWAJI WA KANUNI

Kwa: M/s ............................................................ mwenye usajili na. ...............................................

Kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania, Sura ya 415 na Kanuni za Usajili wa Wasafirishaji kwa Njia ya Maji, 2023 ninakutaka kurekebishe mapungufu /ukiukwaji wa kanuni ndani ya siku.................................................................... kama ifuatavyo:

(1) ...............................................................................................................
(2) ...............................................................................................................
(3) ...............................................................................................................

Kushindwa kurekebisha mapungufu/ukiukwaji wa kanuni ulioonekana ndani yamudauliotajwahapojuu,Shirika litalazimika....................................................

Mahali................................. tarehe……… mwezi .................... 20...........

*Tangazo La Serikali Na. 384 (Linaenedelea)*

……………………………………..
MKURUGENZI MKUU
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA

Dodoma
18 Mei, 2023

MAKAME M. MBARAWA
*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi*